FAHAMU KUHUSU HUDUMA YA MAJITAKA NA MIPANGO YA DAWASCO KUBORESHA MIFUMO YA MAJITAKA

Kwa upande wa Huduma ya Majitaka ni **10%** tu ya wakazi wa jiji pekee ambao wameunganishwa katika mtandao wa Majitaka. Mfumo huu ni wa muda mrefu ambapo ulijengwa kati ya miaka **1950 – 1970** hali inayopelekea kuzidiwa na hivyo huziba mara kwa mara kutokana na uchakavu.

Maeneo yenye mfumo wa Majitaka kwa sasa yanayohudumiwa na DAWASA ni **City center , Kariakoo , Upanga , Mikocheni , Regent Estate , Kijitonyama , Buguruni , Pugu road , Tazara , Ubungo , Lugalo, Airwing, pamoja na Mgulani**.

Namna ambavyo Majitaka huzalishwa;

Uzalishaji wa Majitaka unatofautiana na ule wa Majisafi. Wakati uzalishaji wa Majisafi unaanza kwenye chanzo na kuishia kwa watumiaji, Majitaka yananza kwa watumiaji na kuishia mabwawani kabla ya kutibiwa na kuachiwa kwenye mfereji wa wazi ili yaelekee baharini.

Mfumo wa Majitaka unaanzia kwenye ukusanyaji (Collection) toka kwenye mfumo wa mabomba ya Majitaka au chemba zilizokuwa zinahifadhi Majitaka hayo. Hatua hii ya kwanza ni muhimu kwani chemba za Majitaka na mabomba hukusanya uchafu wote wa Majitaka na kuyahifadhi ili kusafisha kwa wakati husika.

Baada ya ukusanyaji kufanyika, hatua nyingine inayofuata ni usafirishaji (Transportation) wa Majitaka, kutoka kwenye mabomba madogo ya wateja (laterals) kwenda kwenye mtandao mkuu na kuishia mabwawani (Waste Stabilization Ponds, WSP's) au baharini kwa maeneo ya Upanga, Kariakoo and City Centre. Hatua hii hufanywa na DAWASCO kwa wale waliounganishwa kwenye mtandao wa Majitaka, au na watu binafsi wenye magari ya kumwaga Majitaka, ambayo ni maalum kwa watu ambao hawajaunganishwa na mtandao wa Majitaka katika maeneo yao au viwandani.

Hatua ya tatu baada ya usafirishaji ni kutibu Majitaka (Treatment). Majitaka hutibiwa kwa kutumia njia ya asili (Biological treatment) ambayo inatumia bacteria wa asili kusafisha Majitaka hayo kwa kupitisha kwenye mabwawa (Waste Stabilization Ponds) ambayo yana sifa na kina tofauti ili kurahisisha usafishaji huo. Kudumu kwa bacteria hawa kutategemea sana aina ya Majitaka yanayomwaga.

Iwapo Majitaka yenye sumu yatamwaga, mfano Majitaka ya viwandani, zoezi la kutibu Maji haya huwa gumu kwani bacteria hawa watakufa hivyo kusababisha Maji yatakayotoka bwawa la mwisho kuwa na sumu na kusababisha viumbe hai wa kwenye mito kama samaki,vyura n.k kufa.Kutokana na tatizo hili, iwapo maeneo ya viwandani yanahitaji huduma ya Majitaka, ni lazima Maji wanayozalisha yapelekwe maabara ya serikali ili kuhakiki kama Majitaka yao yanaruhusu kumwaga kwenye mabwawa yetu kwa ajili ya kuwalinda bacteria walioko.

Iwapo itagundulika yana sumu,watashauriwa kuwa na utibuji wa mwanzo (Primary treatment) kwenye eneo lao ili kuondoa sumu, kabla hayajaleta kwenye mfumo wa DAWASCO.

DAWASA pamoja na DAWASCO imeanza kufanya jitihada za makusudi za kuhakikisha wakazi wote wa jiji la Dar es salaam wanaunganishwa katika mtandao wa Majitaka.

Kwa kuzingatia ukuaji wa kasi wa jiji la Dar es salaam, serikali imebuni mpango wa muda wa kupanua mtandao wa Majitaka kutoka 10% za sasa hadi 30% miradi itakayohusika katika mpango ni pamoja na upanuzi wa mtandao wa Majitaka maeneo ya **Kinondoni, Hananasif, Mwananyamala, Tandale, sinza na Makumbusho** sambamba na mitambo mitatu ya kisasa ya kutibu Majitaka itakayojengwa maeneo ya **Jangwani, Kurasini na Mbezi Beach**.

Serikali kupitia Wizara ya Maji na Umwagiliaji, inakamilisha taratibu za kifedha na serikali ya Korea Kusini na Benki ya Dunia kwa ajili ya kutekeleza miradi ya upanuzi wa mtandao wa Majitaka maeneo hayo ya Jangwani na Mbezi Beach.

Mikakati ya DAWASCO katika kuboresha mifumo ya Majitaka

- Kuongeza mitandao ya Majitaka katika maeneo mbalimbali ambayo hayana mtandao huo wa Majitaka
- Kuongeza wateja wapya kwenye mfumo wa Majitaka ili kukidhi idadi ya wateja pamoja na kupunguza malalamiko yanayohusiana na ukosekanaji wa mtandao wa Majitaka
- Ukarabati na matengenezo ya mfumo wa Majitaka ikihusisha kuongeza ukubwa wa mifereji mikuu ya Majitaka, kubadilisha mifuniko iliyopasuka kuibwa na kuweka mifuniko mipya ili kupunguza umwagikaji ovyo wa Majitaka mitaani.

- Utoaji wa tope, taka ngumu na ukataji wa majani kwenye mabwawa ili kuongeza ufanisi katika mabwawa kutibu Majitaka.

Changamoto inayoikabili Dawasco katika kuboresha mtandao wa Majitaka

- Ukosefu wa miundombinu ya Majitaka ya kutosha
- Uchakavu wa Miundombinu ya Majitaka
- Uhujumu, uharibifu na matumizi mabaya ya miundombinu ya Majitaka
- Kupasuka mara kwa mara kwa mabomba ya Majitaka.
- Wizi wa miundombinu ya Majitakahususani mifuniko ya chemba za majitaka ambazo hufanywa kama chuma chakavu.
- Matumizi mabaya ya chemba za Majitaka, Wananchi wengi hutumia chemba hizo kutupa taka ngumu inayopelekea kujaa kwa chemba hizo za Majitaka

Hivyo ni muhimu wananchi wakajua kuwa miundombinu ya Majitaka ni yao hivyo wanahusika kuilinda kwa namna mbalimbali ya uhujumu ili kuzuia kero za mara kwa mara ikiwemo kutiririka kwa Majitaka ovyo, Kutotupa taka ngumu katika mabwawa ya Majitaka pamoja na kutoa taarifa kwa mamlaka ya DAWASCO pindi chemba na mabwawa ya Majitaka yanapoziba au mifuniko ya chemba ya Majitaka inapoibiwa .

Kwa maelezo juu ya huduma za Majisafi na Majitaka kwa jiji la Dar es salaam tafadhali wasiliana na kituo chetu cha huduma kwa wateja 0800110064 (**BURE**).